# WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

# SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO

**Reg. No. S.0576**

**Mob: 0762818180/0754636049/0621064022/0718057333**
**Website:** www.ruhuwikoschools.ac.tz
**Email:** ruhuwikosecschool@gmail.com

**S.L.P. 448,**
**SONGEA.**

**Tarehe: ……………………………**

**JINA LA MWANAFUNZI: ……………………………………………………………………………………**

## YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS) KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA 2022.

### 1.0. UTANGULIZI

Napenda kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Ruhuwiko **KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2022.**

1.1. **Kufungua Shule**

Shule itafunguliwa tarehe **10/01/2022 kwa wanafunzi wote.** Wanafunzi wa bweni waripoti tarehe **08/01/2022** na **09/01/2022**. Fika na mahitaji yote muhimu ili uweze kusajiliwa na kuanza Masomo Rasmi.

1.2. **Mahali Shule Ilipo**

Shule ya Sekondari Ruhuwiko ipo katika eneo la JWTZ Kikosi cha Jeshi cha Huduma (411 KJ) katika Manispaa ya Songea barabara iendayo Wilaya ya Mbinga.

### 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

**Ufikapo shuleni unatakiwa kuripoti ofisi ya usajili kwa maelekezo ukiwa na nyaraka zote muhimu kama:-**

2.1 Fomu ya Maombi *(Application Form)* na Picha ndogo *(Passport size 1)*

2.2 Nakala ya Cheti cha kumaliza elimu ya Msingi au Barua kutoka kwa Mwalimu Mkuu inayothibitisha kuwa ulisoma shule hiyo ikionesha Namba ya Mtihani wa Darasa la Saba.

2.3 Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa na Fomu ya Vipimo vya Afya.

### 3.0. ADA YA SHULE

Malipo ya ada ya shule ya Muhula husika yanafanyika kila mwanzo wa Robo muhula (Kwa Mara moja) na yalipwe kupitia benki tu kwenye **A/C No. 023101000790 NBC**, **A/C No. 01J1085291000 CRDB** au **A/C No. 61803500130 NMB**. Jina la akaunti ni **MKUU WA SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO. Unapolipa ada andika Majina ya Mwanafunzi kwenye risiti ya Benki (**Original Pay in Slip**)** iletwe Shuleni. Hakuna malipo yoyote ya fedha taslimu yanayopokelewa shuleni, **ISIPOKUWA FEDHA ZA SARE NA BIMA YA AFYA ZILETWE TASLIMU (CASH).**

### 4.0. MGAWANYO ADA YA SHULE

| ADA KWA WANAFUNZI WA BWENI | | ADA KWA WANAFUNZI WA KUTWA | |
|---|---|---|---|
| **Januari - Machi** | **- Tshs. 350,000/=** | **Januari - Machi** | **- Tshs. 250,000/=** |
| **Aprili - Juni** | **- Tshs. 340,000/=** | **Aprili - Juni** | **- Tshs. 230,000/=** |
| **Julai – Septemba** | **- Tshs. 350,000/=** | **Julai – Septemba** | **- Tshs. 250,000/=** |
| **Octoba - Desemba** | **- Tshs. 340,000/=** | **Octoba - Desemba** | **- Tshs. 200,000/=** |
| **Kwa Mwaka** | **Tshs. 1,380,000/=** | **Kwa Mwaka** | **Tshs. 930,000/=** |

***ZINGATIA: ADA IKILIPWA HAIRUDISHWI***

### 5.0. SARE (UNIFORMS)

Mwanafunzi **huruhusiwi** kujishonea Sare za Shule. Sare zote zinashonwa shuleni kwa gharama zifuatazo:-

**a) Wavulana**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Suruali mbili | Tsh. 35,000/= |
| ii. | Sweta lenye nembo | Tsh. 17,000/= |
| iii. | Fulana 1 (T-shirt 1) yenye nembo | Tsh. 15,000/= |
| iv. | Nguo za kazi *(shamba dress) jozi 1* | Tsh. 32,000/= |
| v. | Tai moja | Tsh. 2,000/= |

**Jumla ya Gharama za Sare**
**Wavulana wa Bweni – Tshs. 101,000/=**
**Wavulana wa kutwa – Tshs. 69,000/=**

b) **Wasichana**

i. Sketi mbili Tsh. 35,000/=
ii. Sweta lenye nembo Tsh. 17,000/=
iii. Fulana 1 (T-shirt 1) yenye nembo Tsh. 15,000/=
iv. Nguo ya kazi – gauni 1 *(shamba dress)* Tsh. 26,000/=
v. Tai moja Tsh. 2,000/=

**Jumla ya Gharama za Sare**

**Wasichana wa Bweni – Tshs. 95,000/=**

**Wasichana wa kutwa – Tshs. 69,000/=**

c) **Mzazi/mlezi mnunulie mwanao:-**

i. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
ii. Nembo ya shule ya kushona kwenye shati 2x4,000/- = 8,000/= (cash)
iii. Viatu vyeusi vya Kamba
iv. Soksi nyeusi na mkanda mweusi kwa wavulana na soksi nyeupe kwa wasichana.

## 6.0. BIMA YA AFYA

Kila Mwanafunzi anatakiwa kuja na **Bima ya Afya** na kwa wale ambao hawana wanatakiwa kuja na **Fedha Taslimu (Cash)** **Tshs. 50,400/=** kwa ajili ya kukatiwa bima ya Afya.

## 7.0. VIFAA VYA DARASANI NA MAZINGIRA

a. Vitabu vya masomo ya darasani **ni lazima kwa kila Mwanafunzi**. *(Orodha imeambatanishwa)*
b. Kamusi *(Advanced Dictionary – English to English)* moja kubwa na Atlasi.
c. Daftari kubwa *(Counter Books)* – 12 pamoja na Begi la kubebea daftari.
d. Bunda la Karatasi za kurudufu *(Ream - $A_4$)* bunda moja kila mwanzo mwa muhula mpya.
e. Fagio la mpira la kudekia – mopa *(Rubber squeeze) - 1*
f. Ndoo moja ya plastiki ya lita 20.
g. Jembe moja lenye mpini.
h. Fagio laini ndefu 1, Brashi ngumu fupi 1.
i. Fyekeo/kwanja, Ufagio wa chelewa 1.
j. Kila mwanafunzi awe na **Saa ya Mkononi** na Kitambaa ***(Leso)*** cheupe.

## 8.0. VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI WA BWENI

a. Nguo za michezo **(Tracksuit Rangi Nyeusi**, fulana nyeusi, bukta nyeusi na raba ya michezo.
b. Shuka mbili rangi ya bluu bahari, Blanketi 1 , Mto 1, na Godoro moja la futi $2^1/_2$
c. Sanduku imara la chuma na Kufuli.
d. Chandarua (mosquito net) 1.
e. Ndoo ndogo ya kuogea, Taulo na Kandambili.
f. Vyombo vya kulia chakula *(Kontena, Kikombe na Kijiko).*
g. Kanga mbili kwa wasichana na Vitu vidogovidogo kwa matumizi yake binafsi.

## 9.0. NGUO MAALUMU ZA KUVAA BAADA YA VIPINDI *(SHAMBA DRESS)*

Wanafunzi bweni wanavaa nguo za kazi baada ya muda wa masomo na siku zote ambazo sio za masomo *(weekend days)*. Utaratibu huu ni **wa lazima** kwa kila mwanafunzi wa bweni ili kudumisha nidhamu, kuondoa vishawishi vya wizi wa mavazi ya nyumbani na tabia nyingine mbaya zinazoambatana na uvaaji wa nguo za nyumbani. Mvulana atashonewa na shule shati na suruali jozi moja na msichana atashonewa na shule gauni la heshima (refu). **Nguo za nyumbani haziruhusiwi** na ukaguzi unafanywa mara mwanafunzi anapofika Shuleni.

**10.0.** a) **Wastani wa Shule**: Mwanafunzi anaruhusiwa kuendelea kidato cha pili, tatu au cha nne iwapo amepata **wastani wa kuanzia 50%** na kuendelea katika masomo yake yote mwisho wa mwaka.

b) **Simu haziruhusiwi kabisa kwa wanafunzi**: Mwanafunzi atakayekamatwa na simu hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuchoma simu na mwanafunzi kusimamishwa shule

c) **Sheria za Shule:-** Kila Mwanafunzi atapewa nakala ya Sheria za Shule na anatakiwa kufuata sheria zote za shule zilizowekwa kikamilifu pamoja na taratibu nyingine atakazoelekezwa.

**KARIBU SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO UPATE ELIMU BORA, MALEZI BORA NA NIDHAMU THABITI**

……………………………………

**Mkuu wa Shule**